



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA



Kumb. Na.LD/MK/8690/9
Mkurugenzi Mtendaji
Kituo cha Uwekezaji Tanzania
S.L.P.838
Dar Es Salaam.

25/6/2024



YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA KIGENI KUNUNUA KIWANJA
NA.9 BLOCK 'J' DUNDANI, WILAYA YA MKURANGA


Rejea mada tajwa hapo juu

Ninachukua fursa hii kujulisha Ofisi yako kwamba, **Biobuu Limited** ya S.L.P.80394 **Dar es salaam** imenunua kiwanja Na.9 kitalu 'J' **Dundani** ambacho kimetokana na upimaji wa eneo lililonunuliwa na kisha kupangwa na kupimwa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, fungu la 20 sambamba na fungu la 12 & 179 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, Kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C (v) na Sheria ya uwekezaji Tanzania Na. 26 ya 1997, kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Naambatanisha nyaraka za usajili wa kampuni ,ramani ya mipango miji, ramani ya upimaji Mkataba wa kupata Ardhi, uthibitisho wa uraia wa wawekezaji, MoU and Articles of Association, na nyaraka zote muhimu kwa ajili ya mchakato wa usajili wa mwekezaji na utaoaji wa Certificate of Incentive kabla ya ugawaji wa kiwanja hiki ngazi ya kamati ya Ardhi ya Taifa.

Naomba kuwasilisha.


Chagiye R.M
K.n.y: Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga.

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W).

Mkuranga

-Kwa taarifa

Biobuu Limited

S.L.P.80394 **Dar es salaam** -Kwa taarifa na ufuatiliaji usajili TIC